



Na.21: Msimu wa Kilimo 2025/26

Tathmini ya Aprili 21-30, 2026 na Matazamio kwa Kipindi cha Mei 1-10, 2026

### MUHTASARI

- Mvua zinazotarajiwa katika maeneo machache ya nchi zitasaidia kuimarisha unyevu wa udongo, hivyo kusaidia katika ukuaji wa mazao na upatikanaji wa malisho.
- Hali ya ukavu inayotarajiwa hususan katika mkoa wa Singida itasaidia katika ukuaji wa zao la alizeti ambalo lipo katika hatua ya kukomaa.
- Wakulima na wadau wa kilimo wanashauriwa kushirikiana na maafisa ugani katika maeneo yao, sambamba na kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa kwa mipango thabiti ya shughuli za kilimo.


### MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2026

**K**atika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilipungua nguvu. Hali hii ilisababisha ukanda mvua kusogea kuelekea kaskazini na kuwepo katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, magharibi mwa nchi, nyanda za juu kaskazini mashariki na ukanda wa pwani, na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo. Aidha, upepo wa bahari wenye unyevunyevu uvumao kutoka mashariki na kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo jirani uliendelea kuimarisha zaidi mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, nyanda za juu kaskazini mashariki, magharibi mwa nchi na ukanda wa pwani; na vipindi vya mvua katika maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi na kanda ya kusini. Aidha, vipindi vya mvua kubwa viliripotiwa katika maeneo ya ukanda wa pwani na nyanda za juu kaskazini mashariki.

### TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2026

**K**atika dikadi hii, maeneo mengi ya nchi yalipata kiasi cha mvua cha kati ya milimita 10 hadi 50. Kiasi kikubwa zaidi cha mvua cha dikadi, cha kati ya milimita 101 hadi 150, kilirekodiwa katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, nyanda za juu za kaskazini-mashariki pamoja na maeneo ya Pwani ya kaskazini. Hata hivyo, baadhi ya maeneo machache katika kanda ya kati (Dodoma na Singida), nyanda za juu za kusini-magharibi (Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), pamoja na kanda ya kusini (Ruvuma) yalipata hali ya ukavu kwa kiasi, kama inavyoonyeshwa katika Kielelezo.



Kielelezo 1: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Aprili 21-30, 2026

### TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2026

**K**atika kipindi hiki cha dikadi, maeneo mengi ya nchi, hususan kanda ya Ziwa Victoria, nyanda za juu za kaskazini mashariki na pwani ya kaskazini, yalipata mvua zilizoongeza unyevunyevu kwenye udongo na kusaidia katika ukuaji wa mazao. Hata hivyo, kulijitokeza kutuama kwa maji katika baadhi ya maeneo ya mabondeni, hususan katika maeneomachache ya pwani ya kaskazini.

Katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua, hususan pwani ya kaskazini, kanda ya Ziwa Victoria na sehemu za nyanda za juu za kaskazini mashariki, mahindi yalikuwa katika hatua za ukuaji wa majani hadi kutoa mahindi, na wakulima waliendelea na shughuli za kawaida za shambani kama kunyunyizia dawa za kuua wadudu.

Katika mkoa wa Morogoro, zao la mpunga lilikuwa katika hatua ya kutoa maua, na katika mkoa wa Mwanza, Mbeya na Rukwa lilikuwa katika hatua ya kukomaa.

Kwa maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua, zao la mahindi lilikuwa katika hatua ya ukomavu wa nta, ingawa katika mkoa wa Tabora yalikuwa tayari yamekomaa na baadhi ya wakulima walikuwa wameanza kuvuna.

Kwa upande wa mazao ya kudumu, kama kahawa katika mikoa ya Kilimanjaro na Songwe, yalikuwa katika hatua ya tunda laini, huku karafuu katika visiwa vya Pemba zikiwa katika hatua ya “makonyo”. Hali nzuri ya unyevunyevu wa udongo iliokuwepo iliendelea kusaidia katika ukuaji wa matunda ya karafuu, na wakulima waliendeleza shughuli za uangalizi wa mashamba.

Upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo na wanyamapori uliendelea kuimarika katika maeneo mengi yaliyopata mvua za kutosha, hali iliyochangia kuboresha upatikanaji wa malisho.

### HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2026

**K**wa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito kiliongezeka hususan kwa maeneo ambayo yalipata mvua.

### MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 1-10, 2026

**K**atika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kupungua nguvu. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda mvua kusogea kuelekea kaskazini na kuwepo katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, nyanda za juu kaskazini mashariki na ukanda wa pwani, na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

Aidha, mifumo ya hali ya hewa iliyopo katika ukanda wa Ziwa Victoria inatarajiwa kuimarika pamoja na upepo wa bahari wenye unyevunyevu uvumao kutoka mashariki na kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani vinatarajiwa kuendelea kuimarisha zaidi mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

### HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 1-10, 2026

**M**aeneo ya kanda ya ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), pwani ya kaskazini (Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) yanatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

Pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) yanatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) yanatarajiwa kupata vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) kunatarajiwa kupata mvua katika maeneo machache.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), kanda ya kusini (Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro), kunatarajiwa kupata vipindi vya mvua katika maeneo machache.

Kanda ya kati (Dodoma na Singida) kunatarajiwa kuwa na hali ya ukavu kwa ujumla.

### HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA MEI 1-10, 2026

**H**ali ya mvua inayotarajiwa katika maeneo mengi nchini itaendelea kusaidia kuongeza unyevu nyevu katika udongo na kusaidia ukuaji na maendeleo ya mazao. Hali ya ukavu inayotarajiwa hususan katika mikoa ya Dodoma na Singida inatarajiwa kusaidia maendeleo ya zao la alizeti lilipo katika hatua ya kutoa maua na kukomaa.

#### Ushauri:

- **Maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua (kanda ya Ziwa Victoria, Pwani ya Kaskazini na Nyanda za juu Kaskazini Mashariki):** Wakulima katika maeneo haya wanashauriwa kuchukua tahadhiri kutokana na uwepo wa magonjwa na wadudu waharibifu wa mazao na kupulizia dawa mara tu itakapohitajika. Pia wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku kwa mipango thabiti ya shughuli za kilimo.
- **Maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua (Nyanda za Juu Kusini Magharibi, Mikoa ya Magharibi, Pwani ya kusini na Kanda ya Kati na Kusini):** Wakulima wanashauriwa kufuatilia hali ya mazao na pia kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku.
- **Malisho na upatikanaji wa maji kwa wafugaji:** Wafugaji wanashauriwa kuendelea kupanda majani ya malisho na kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.
- **Wavuvi wa Samaki baharini na maziwa makuu:** Wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku ili kujua wakati sahihi wa kufanya shughuli za uvuvi kutokana na uwezekano wa kujitokeza mawimbi makubwa na upepo mkali

Ushauri huu umedhamiria kuongeza tija kwenye kilimo na kupunguza athari zitokanazo na hali mbaya ya Hewa. Wadau wote wa kilimo wanahimizwa kufuatilia taarifa za hali ya hewa ili kuwa na mipango thabiti ya shughuli za kilimo.

### HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 1-10, 2026

**K**ina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kubaki kawaida katika maeneo mengi. Jamii inashauriwa kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.